

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W) LUNGUYA MTWANGO KWA TAREHE 29/10/2021

WAJUMBE WA BODI WALIOHUDHURIA:

S/N	JINA	CHEO	WADHIFA
1.	Ahmadi Maguo	DNRO	Mwenyekiti
2.	Matio O. Nkomola	DPSO	Katibu
3.	Augustino M. Nyenza	DLFDO	Mjumbe
4.	Anganile Daniel	DPLO	Mjumbe
5.	John Ndumbalo	DEO (S)	Mjumbe
6.	Adv. George Makacha	DLO	Mjumbe
7.	MahamuduKankwanzi	DEO (P)	Mjumbe

SECRETARIET WALIOHUDHURIA:

S/N	JINA	CHEO
1.	AthumanMgata	SO
2.	ThobiasMwandikile	SO

WAGENI WAALIKWA:

S/N	JINA	CHEO
1.	GhristopherHaule	AfisaElimuTaaluma H/W
2.	Livin John	AfisaUtarwalaUtumishi
3.	Fadhili Mungure	KaimuMhandisiUjenzi H/W
4.	Angela Barasa	AfisaElimuVifaanaTakwimu H/W

Agenda za Kikao.

1. Kufungua Kikao
2. Kupokea Agenda
3. Mapendekezo ya matumizi ya Force Account katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inaayofadhiriwa na serikali kuu kuitia program ya fedha za UVIKON -19 .
4. Mengineyo
5. Kufunga Kikao.

MUHTASARI NO. 01/10/2020 - 2021 KUFUNGUA KIKAO

- 1.1 Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya ufunguzi wa kikao aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwajulisha kuwa akidi ya Wajumbe imetimia na kuwa katika kikao hicho kuna wageni waalikwa ambao

wamealikwa kutokana na Agenda zitakazojadiliwa kuhitajika ufanuzi toka kwa wajumbe hao ili kuiwezesha Bodi ya Zabuni kufikia maamuzi sahihi kwa agenda zitakazowasilishwa na kujadiliwa.

- 1.1.1 Baada ya maelezo hayo Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kwa ufunguzi wa kikao.
- 1.1.2 Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe wa Bodi, wageni waalikwa na Sekretarieti kwenye kikao na kuwataka kuchangia mawazo yao ili kuweza kufikia maamuzi sahihi kwa kila Agenda itakayojadiliwa.
- 1.1.3 Mwenyekiti alifungua Kikao saa nne na dakika arobaini na tano Asubuhi (4:45)

MUHTASARI NO 02/06/2020 – 2021 KUPOKEA AGENDA

- 2.1 Jumla ya Agenda tano ziliwasilishwa kwa wajumbe na kupokelewa kwa ajili ya majadiliano.

MUHTASARI NO. 3/10/2020 – 2021 MAPENDEKEZO YA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAA YOFADHIRIWA NA SERIKALI KUU KUPITIA PROGRAM YA FEDHA ZA UVIKON -19

- 3.1.1 Ilifahamishwa kuwa Idara ya Elimu Msingi imepokea fedha kiasi cha Tsh. 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Shule Shikizi mbili (2), Shule ya Msingi Itova na Shule ya Msingi Shikizi Tembeli kila Shule imetengewa kiasi cha Tshs. 40,000,000.00 na kwa upande wa Idara ya Elimu Sekondari imepata fedha kiasi cha Tsh. 480,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ishirini na nne (24).
- 3.1.2 Pia kwa upande wa Idara ya Afya ilipokea kiasi cha Tsh. 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 IN 1) Zahanati ya Ninga ambapo jumla ya fedha kiasi cha Tsh. 650,000,000.00 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kupitia program ya UVIKO -19 kwa utaratibu wa Force account.
- 3.1.3 Katika mwongozo huo walianisha makampuni mawili ya usambazaji wa bati ambayo ni **ALAF Limited** na **MMI Intergrated Steel Mills** ambayo ya na gharama na fuu ili kampuni hizi zitumike kwa kila Halmashauri kuweza kusambaza bati hizo.

- 3.1.4 Wajumbe walijadili kuwa utaratibu waupatikanaji wa mafundi utatumika kwa kuwa shirikisha mafundi wazawa (Local Fund) katika utekelezaji wa miradi hiyo ili kuweza kupata gharama nafuu za ujenzi.
- 3.1.5 Wajumbe kwa Pamoja waliridhia utaratibu wa Force account katika utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa kuhusisha ushindanishi wa kotesheni za vifaa vya ujenzi kwa wazabu niwaza wana viwanda ili kupata vifaa vyenye ubora utakaosaidia kupata thamani halisi ya fedha (Value for Money).

MUHTASARI NO. 04/10/2020 – 2021 MENGINEYO

- 4.1 Hapakuwa na Mengineyo mezani kwa Mwenyekiti.

MUHTASARI NO. 05/10/2020 – 2021 KUFUNGA KIKAO

- 5.1 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano wao kwenye kikao hicho na michango yote ya mawazo.
- 5.1.1 Mwenyekiti aliwaomba sekretarieti na Idara ya ujenzi kushirikiana kwa Pamoja katika utekelezaji wa miradi hiyo ya ujenzi kushirikiana na Idara ya Secretariat kufuatilia majibu ya maazimio yote yalivitolewa.
- 5.1.2 Mwenyekiti alifunga kikao saa 6.05 Mchana.

Imethibitishwa

Ahmad Maguo
Mwenyekiti
Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Wilaya
Njombe

Matia O. Nkomola
katibu
Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Wilaya
Njombe